Je wewe ni miongoni mwa waliochaguliwa sawasawa na andiko hili?…

> *Waefeso 1:11 ”na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake”.*

Kama wewe ni miongoni mwa waliochaguliwa basi fahamu lengo/kusudi la kwanza la wito wa MUNGU kwako ni lipi?..

Hebu tuusome wito wa Mtumishi wa Mungu Paulo, tuweze kujua nia ya Kristo ipi…

> *Matendo 22:13 “Akanijia, akasimama karibu nami, akaniambia, Ndugu yangu Sauli, uone. Nikamwinulia macho yangu saa ile ile.*
>
> *14 Akasema, Mungu wa baba zetu amekuchagua wewe upate KUJUA MAPENZI YA MUNGU, na kumwona yule Mwenye haki, na kuisikia sauti itokayo katika kinywa chake”.*

Hapo anasema *“Mungu wa baba zetu amekuchagua wewe upate kujua MAPENZI YAKE..”.*..Jiulize kwanini ataje jambo la kwanza “mapenzi ya Mungu”.

Kumbe lengo la kwanza la Mungu kumwita Paulo ni yeye *“kuyajua mapenzi ya Mungu”.* Na mengine ndiyo yafuate..

Na ni sahihi kabisa kwani Bwana YESU mwenyewe alituambia maneno yafuatayo…

> *Mathayo 7:21 “Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye AFANYAYE MAPENZI YA BABA YANGU ALIYE MBINGUNI”.*
>
> *22 Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?*
>
> *23 Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu”*

Umeona?..kwahiyo kumbe Bwana anataka tuyajue sana mapenzi yake na tuyafanye..

Je unayajua mapenzi ya Mungu??…na je unayafanya pia?.

Mapenzi ya MUNGU ni haya…

> *1 Wathesalonike 4:3 “Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati;*
>
> *4 kila mmoja wenu ajue kuuweza mwili wake katika utakatifu na heshima;*
>
> *5 si katika hali ya tamaa mbaya, kama Mataifa wasiomjua Mungu”.*

1. Utakaso ni sehemu ya mapenzi ya MUNGU kwako.

*(Na unatakasika kwa maombi, mifungo, kusoma Neno, na kuhudhuria ibada).*

2. Pia Kuuweza mwili katika utakatifu na heshima ni sehemu ya mapenzi ya MUNGU kwako.

(Maana yake mwili wako kuuweka katika hali ya heshima, ikiwemo kuvaa mavazi ya heshima na staha, ikiwemo kutojichubua, na kutofanya uasherati na mambo yote yanayohusika kuuchafua mwili”.

Yajue mapenzi ya MUNGU, yafanye mapenzi ya MUNGU.

Kwa urefu zaidi kuhusu Mapenzi ya MUNGU fungua hapa□□MAPENZI YA MUNGU NI YAPI?

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP,

jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>
https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp